

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

*Simu:* +255 026 23222761-5  
*Fax No.* +255 026 2322624  
**E-mail:** [info@bunge.go.tz](mailto:info@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA**

**TAARIFA KWA UMMA**

---

Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Ndugai amemuandikia barua Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Mheshimiwa Jaji Semistocles Kaijage kumfahamisha kuwa Majimbo ya Kinondoni na Siha yapo wazi baada ya waliokuwa Wabunge wa Majimbo hayo Ndg. Maulid Said Abdalah Mtulia (CUF) na Ndg. Dkt. Godwin Aloyce Mollel (CHADEMA) kumwandikia barua ya kuacha uanachama na Ubunge.

Mheshimiwa Spika ameandika barua hiyo kwa mujibu wa kifungu 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi (Sura ya 343, ya mwaka 2015) kinachoeleza kwamba, pale ambapo Mbunge, atajiuzulu, atakufa au sababu nyingine yoyote tofauti na zilizoainishwa katika kifungu cha 113, Spika atamuandikia barua Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali kwamba viti hivyo vya Ubunge viko wazi.

Kufuatia barua hiyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaweza kuendelea na mchakato wa kuwapata Wabunge wa kujaza nafasi hizo zilizo wazi za Majimbo ya Kinondoni na Siha.

**Imetolewa na;** Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano,  
Ofisi ya Bunge  
S.L.P 941,  
**DODOMA.**

15 Desemba, 2017.